



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA**  
**WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI**  
**(RITA)**



**SHERIA YA USAJILI WA WADHAMINI SURA YA 318 TOLEO LA 2002**

**TANGAZO KWA BODI ZA WADHAMINI WA TAASISI**  
**ZILIZOSAJILIWA KATIKA OFISI YA KABIDHI WASII MKUU/RITA**

1. KABIDHI WASII MKUU (ADMINISTRATOR GENERAL) ANAWATANGAZIA WADHAMINI WA TAASISI/ASASI ZOTE ZILIZOSAJILIWA NA OFISI YA KABIDHI WASII MKUU/RITA KUFANYA MAREJEO YA KATIBA ZA TAASISI ZAO KWA KUFANYA MAREKEBISHO ILI KUONGEZA/KUBORESHA YAFUATAYO :-
  - i. KUWEKA IBARA INAYOAINISHA CHOMBO CHA JUU CHA TAASISI HUSIKA (SUPREME AUTHORITY) KWA TAASISI ZA KIDINI;
  - ii. KUWEKA IBARA INAYOELEZEA NAMNA YA UTATUZI WA MGOGORO/MIGOGORO INAPOTOKEA KWENYE TAASISI;
  - iii. KUWEKA IBARA INAYOONESHA MUDA WA UKOMO WA WADHAMINI KUKAA MADARAKANI;
  - iv. KUWEKA IBARA INAYOONESHA SABABU ZA MDHAMINI/WADHAMINI KUONDOKA/KUONDOLEWA MADARAKANI;
  - v. KUWEKA IBARA INAYOONESHA IDADI YA VIKAO VYA WADHAMINI KWA MWAKA NA MAJUKUMU YAKE IKIWA PAMOJA NA WAJUMBE WANAOPASWA KUHUDHURIA VIKAO HUSIKA NA AKIDI (QUORUM) KWA VIKAO;
2. AIDHA TAASISI/ASASI ZILIZOSAJILIWA OFISI YA MSAJILI WA JUMUIYA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI NA ZINAPASWA KUSAJILI BODI ZA WADHAMINI RITA LAKINI HAZIJAFANYA HIVYO ZINAPASWA KUFANYA HIVYO KWA MUJIBU WA SHERIA. VILEVILE BODI ZA WADHAMINI WA TAASISI ZA KIDINI AMBAZO HAZIKUSAJILIWA MAMBO YA NDANI ZINAELEKEZWA KUFANYA HIVYO.

IZINGATIWE KWAMBA mnatakiwa kuwasilisha Katiba zikiwa na marekebisho hayo ndani ya siku Tisini (90) tangu tarehe ya kutolewa kwa tangazo hili.

IMETOLEWA hapa Dar es Salaam kwa mkono na sahihi yangu leo hii tarehe 25 Julai 2022.

Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu (RITA)  
S.L.P. 9183,  
DAR ES SALAAM.  
Simu: 022-2924180/181  
Nukushi: +022-2924182  
Tovuti: [www.rita.go.tz](http://www.rita.go.tz)

**ANGELA K. ANATORY**  
**KABIDHI WASII MKUU/ AFISA MTENDAJI MKUU**